BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kumi – Tarehe 28 Februari, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Afya:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

157. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Vijana hususan wanaomaliza elimu kwa ngazi ya vyuo vikuu bado wengi wao wana mtazamo wa kusubiri ajira Serikalini.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya ziada katika kubadilisha fikra za vijana ili waweze kujiamini na kujenga uthubutu wa kujiajiri wenyewe baada tu ya kumaliza elimu zao

katika vyuo vikuu mbali mbali.

(b) Je, takwimu zikoje juu ya kujua idadi halisi ya vijana wanaothubutu na kujiamini katika kujiajiri wenyewe.

(c) Je, mikopo ya wajasiriamali ya Mhe. Rais Dkt. Hussein Mwinyi imeweza vipi kuhamasisha vijana wanaomaliza vyuo vikuu kujiajiri kupitia fursa hiyo.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

149. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika siku za hivi karibuni maeneo ya Jiji la Zanzibar yameripotiwa kuwa na ongezeko kubwa la omba omba na kuibuka vikundi vya watu wanaowatumikisha watu wenye ulemavu kuomba. Jambo hili linaleta aibu kwa Jiji na nchi yetu ambayo mambo hayo siyo utamaduni wetu.

(a) Kwa kuwa suala hili limekuwa la muda mrefu, je, Serikali imekuja na mkakati gani wa kuliondoa kabisa kabla hali haijawa mbaya zaidi.

(b) Je, Serikali imefanya uchunguzi wowote ili kuwabaini watu au vikundi vya watu vinavyowatumia baadhi ya watu wenye ulemavu kuomba njiani, na watu hawa wamechukuliwa hatua gani.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

90. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Nyumba ya PBZ iliyopo maeneo ya Mwanakwerekwe imeendelea kubomoka na kutokalika kwa muda mrefu sasa na kwa bahati mbaya haionekani kushughulikiwa.

Je, ni lini nyumba hiyo itafanyiwa matengenezo ili iweze kuleta tija iliyokusudiwa

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

55. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kuna malalamiko ya wananchi kwa kipindi cha muda mrefu sasa kuwa, sanaa yetu haina muelekeo ulio madhubuti. Aidha, Serikali imekuwa ikiendelea kuwatumia wasanii bila kuwafikiria wasanii wenyewe huku kumbi za maonesho ya sanaa zikiendelea kuachwa zikichakaa na kushindwa kuendelezwa ili kuleta tija kwa wasanii na kuwafanya wasanii wafaidike na sanaa yao katika kujikomboa kimaisha.

(a) Je, Serikali imechukua juhudi gani kwa miaka mitano iliyopita za kuboresha na kuziongeza kumbi za maonesho, ili kutoa fursa kwa wasanii kutangaza maonesho yao.

(b) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kulipa uwezo Baraza la Sanaa ili liweze kufanya shughuli zake kwa uwazi na usanifu.

(c) Je, ni upi mpango wa kuyaboresha matamasha ya kimataifa ya maonesho kama vile ZIFF, ili yaweze kuleta tija kwa wasanii wa ndani.

132. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Wananchi wengi wa kizazi cha sasa hawazifahamu nyimbo za muimbaji nguli wa taarab asilia aliyejulikana kwa kuuza kupitia santuri nyimbo zake kutoka Zanzibar hadi mwambao mzima wa bahari ya hindi, maarufu kwa jina la Siti binti Saad.

(a) Je, Wizara yako haioni kwamba kuna haja ya kuzitoa nyimbo hizi ili kuweza kuzirithisha kwa vizazi vipya.

(b) Ni zipi baadhi ya nyimbo hizo kwa faida ya wananchi.

(c) Je, kizazi cha familia ya mwanamuziki huyo nguli wa taarab kipo na kama kipo wanamchango gani katika kuendeleza kumuenzi Siti bint Saad.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

48. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni jambo jema kwamba Serikali imeanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kiafya. Hata hivyo, bado taasisi hii haijawezeshwa kiasi kwamba maabara zake hazijatumika ipasavyo katika kufanya utafiti wa kiafya katika nyanja mbali mbali:

(a) Je, Serikali ina mpango gani bora wa kupata ufadhili kwa ajili ya utafiti wa kiafya na kushirikiana na mashirika ya kimataifa na mataifa yaliyobobea katika tasnia ya afya.

(b) Je, kuna maendeleo gani katika utafiti wa tiba asilia (traditional medicine).

(c) Je, tokea kuanzishwa kwa taasisi hii, ni tafiti ngapi za kiafya na zenye matokeo gani zimefanyika Zanzibar.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

127. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Moja kati ya njia bora na muhimu katika kukikuza na kukieneza kiswahili duniani ni kupitia taasisi mbali mbali za kielimu zinazobeba dhima ya kufundisha kiswahili kwa wageni

(a) Je, TAKILUKI bado inaendelea kutoa huduma hiyo.

(b) Ni mafanikio na changamoto zipi zinazoipelekea TAKILUKI kudorora kutoa huduma hii kwa miaka ya hivi karibuni.

(c) Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kina mikakati gani ya dharura na ile ya muda mrefu ya kuhakikisha kuwa taasisi hii ya TAKILUKI inachukua nafasi kubwa katika kuifundisha lugha yetu adhimu kwa wageni wanaotoka mataifa mbali mbali ili kuweza kuwashinda wenzetu kama vile Kenya.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

93. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na kuendelea kuchimba visima kwa ajili ya kuwapatia maji safi na salama wananchi wetu, katika shehia ya Mgagadu kuna visima vingi ambavyo havitumiki na wala havitoi maji.

(a) Je, Wizara yako imejipanga vipi kuvitumia visima hivyo.

(b) Je, ni lini tutafanya ziara ya pamoja ili ukavione visima hivyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

82. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika sehemu ya kusafiria abiria hapo bandarini Zanzibar palikuwa na TV kwa ajili ya kuangalia abiria wakati wa kusubiria chombo lakini TV hizi hazifanyi kazi kwa zaidi ya miaka minne na baadhi ya TV hizo zimetolewa.

(a) Je, TV zilizotolewa bandarini hapo zimepelekwa wapi.

(b) Kwa nini TV nyingi zilizopo bandarini hapo hazifanyi kazi.

101. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kuangalia mienendo ya meli zetu za ndani na zile za nje zinazopita katika bahari yetu, kuna njia mbali mbali zinazotumika kitaalamu kuongozea meli hizo.

(a) Je, kwa upande wetu hapa Zanzibar tunatumia njia ipi ya kuongozea mienendo ya meli.

(b) Je, katika mwaka wa 2022, ni meli ngapi za nje zilipita ndani ya bahari yetu ya Zanzibar.

(c) Je, meli hizo zilituingizia mapato ya kiasi gani.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

135. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi wengi hususan wakulima wadogo wadogo bado hawajahamasika vya kutosha katika kujikita na kilimo hai.

(a) Je, Wizara yako inachukua mikakati gani juu ya kuwahamasisha wakulima kujikita kwenye kilimo hai.

(b) Je, Wizara inapata changamoto zipi katika jambo hili.

(c) Ni miradi gani maalum kutoka kwa Wizara au wafadhili mbali mbali inayojishirikisha na kilimo hai na wananchi gani ni wanufaika wa miradi hiyo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

154. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Moja ya vivutio vikubwa vya utalii duniani ni kuwepo kwa miji iliyopotea au kuzama baharini kwa miaka mingi na karne nyingi zilizopita.

(a) Je, mji uliopo kwenye Rasi Mkumbuu kisiwani Pemba ni moja kati ya miji hiyo duniani.

(b) Je, Serikali inachukua jitihada gani za kuutangaza kitaifa na kimataifa mji huo wa Rasi Mkumbuu, ili kuliingizia Taifa pato la kigeni.

(c) Je, changamoto gani zisizoweza kutekelezeka ambazo zinarudisha nyuma jitihada za kuutangaza na kufikika kwa urahisi mji huu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Afya:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

Zanzibar,
28 Februari, 2023.

(Raya Issa Msellem)
**KATIBU WA BARAZA.**